AfCHPR
Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510
MUHTASARI WA HUKUMU

IDA AFIAVI AJAVON, JINA WAKATI WA KUZALIWA LIKIWA GOUDJO, NA WENGINE

DHIDI YA

JAMHURI YA BENIN

MAOMBI NA. 063/2019

KUHUMU KUHUSU
MAMLAKA YA KISHERIA NA UKUBALIFU

TAREHE 13 NOVEMBA 2026

UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

Arusha, tarehe 13 Novemba 2026: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) imetoa Uamuzi katika kesi ya *Ida Afiavi Ajavon, jina wakati wa kuzaliwa likiwa Goudjo, na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Benin*.

Tarehe 29 Novemba 2019, Bibi Ida Afiavi Ajavon, jina wakati wa kuzaliwa likiwa Goudjo, Ludmila Isis Ayelé Ajavon na Evaëlle Jonella Noémie Ayoko Ajavon na Bw. Ronald K. Steeven Karen Ayité Ajavon (Waleta Maombi), raia wa Benin wanaoishi Paris (Ufaransa) kama wakimbizi wa kisiasa, waliwasilisha Maombi kwenye Mahakama hii dhidi ya Jamhuri ya Benin (Mjibu Maombi). Waleta Maombi walidai kwamba Mjibu Maombi, kupitia vitendo vyake, alikiuka haki yao ya kumiliki ardhi baada ya Mahakama ya Makosa ya Ukandamizaji wa Kiuchumi na Ugaidi (CRIET) kumhukumu Bw. Sébastien Germain Marie Aïkoué Ajavon, mkurugenzi mkuu na mwanahisa wa COMON SA, kifungo cha miaka ishirini jela. Walidai kwamba akaunti zao binafsi za benki zilitaifishwa kinyume cha sheria na kwamba, kwa nafasi yao kama

wanahisa wa COMON SA, waliathiriwa vibaya na hatua za dhuluma zilizochukuliwa dhidi ya kampuni.

Wanasema kuwa kuna ukiukaji wa haki yao ya kumiliki mali, inayolindwa na Kifungu cha 14 cha Mkataba na haki yao ya kusikilizwa kwa haki, inayolindwa na Kifungu cha 7 cha Mkataba.

Waleta Maombi waliomba Mahakama itumie mamlaka yake na kutangaza kwamba Maombi yanakubalika, ione kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki zao na kuamuru amlipe kila mmoja wao kiasi cha faranga 170,000,000 za CFA kama fidia. Katika Maombi ya ziada yaliyorekebishwa ya tarehe 7 Januari 2020, waliomba tena fidia inayolingana na umiliki wao wa hisa katika kampuni ya COMON, kwa kupoteza fursa katika ushirika wao na PHILIA, pamoja na kiasi kadhaa kwa kupoteza faida, kushuka kwa thamani ya hisa zao katika kampuni ya COMON SA na SOCOTRAC na kupoteza fursa za biashara zinazohusiana na mradi wa mafuta. Pia waliomba amri ya kumtaka Mjibu Maombi alipe gharama zote.

Kwa upande wake, Mjibu maombi aliiomba Mahakama ikatae kutumia mamlaka yake na kutangaza kwamba Maombi hayo hayakubaliki. Vinginevyo, aliomba Mahakama iamue kwamba Maombi hayo hayana msingi na iyatupilie mbali.

Kuhusiana na mamlaka ya kisheria, Mjibu Maombi aliweka pingamizi kuhusu mamlaka ya kisheria ya Mahakama kwa sababu mbili. Kwanza, alidai kwamba Maombi hayo hayaafikiani na Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika na Mkataba na, pili, kwamba hakuna ukiukaji wa haki za binadamu unaodaiwa ndani yake. Kuhusiana na sababu ya kwanza, Mahakama ilibainisha kwamba kuafikiana kwa Maombi na Sheria ya Kikatiba na Mkataba ni takwa la ukubalifu na si suala la mamlaka ya kisheria kushughulikia madai hayo. Kwa hivyo, iliamua kuliangalia katika hatua ya ukubalifu. Kuhusu sababu ya pili, Mjibu Maombi alidai kwamba ukweli tu kwamba Waleta Maombi

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

wanamiliki hisa katika kampuni ya biashara haujumuishi chanzo cha ukiukaji wa haki za binadamu unaoweza kuhusishwa na Serikali.

Mahakama ilirejea hukumu zake za awali kwamba ina mamlaka ya kisheria ya kushughulikia madai haya ilimradi Maombi yanadai kutokea ukiukaji wa haki zilizohakikishwa na Mkataba au hati nyingine yoyote husika ya haki za binadamu iliyoridhiwa na Serikali husika na ikabainisha kwamba Waletaji Maombi walidai kufanyika ukiukaji wa Kifungu cha 14 na 7 cha Mkataba. Kwa hivyo, ilitupilia mbali pingamizi hilo. Kwa kuwa hakuna pingamizi lililowasilishwa kuhusiana na vipengele vingine vya mamlaka ya kisheria, Mahakama ilijiridhisha kwamba mamlaka yake binafsi, ya muda na ya kieneo yalithibitishwa. Kwa hivyo Mahakama ilitangaza kwamba ilikuwa na mamlaka ya kisheria kusilikiliza Maombi.

Kuhusu ukubalifu, Mjibu Maombi alitoa mapingamizi kuhusu Ukubalifu wa Maombi kuhusiana na matakwa ya ukubalifu ambayo hayajatajwa katika Mkataba na Kanuni za Mahakama, akijikita, kwanza, ukosefu wa mada mahususi katika Maombi na athari ya *res judicata* husika na, pili, kuhusiana na matakwa ya ukubalifu yaliyotajwa katika hati hizo, kwa sababu Maombi hayo hayalingani na Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika na Mkataba, kushindwa kukamilisha taratibu za ndani za kisheria na Maombi hayo kutowasilishwa ndani ya muda unaofaa.

Kuhusu suala la ukosefu wa mada mahususi, Mjibu Maombi alidai kwamba hukumu ya fidia ya tarehe 28 Novemba 2019 katika Maombi Na. 013/2017 – *Sébastien Germain Ajavon dhidi ya Jamhuri ya Benini,* tayari ilikuwa imetoa suluhu kikamilifu kuhusu madhara yanayohusiana na COMON SA, ambayo Waleta Maombi ni wanahisa wake. Waleta Maombi walipinga wakisema kwamba fidia iliyotolewa wakati huo ilitoa suluhu tu ya madhara yaliyompata Bw. Sébastien Germain Ajavon mwenyewe na si wao. Mahakama ilibainisha kwamba fidia hiyo ilitolewa kwa Bw. Ajavon yeye binafsi katika nafasi yake kama Mleta Maombi katika kesi hiyo na kwa hivyo haikuweza kufasiriwa kuwa ilikuwa imetoa suluhu ya hasara za kifedha mahususi kwa wanahisa wengine. Iliona kwamba Maombi haya yaliibua suala tofauti, linalohusiana na

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

uwezekano wa kuwepo kwa hasara za kifedha mahususi kwa watu binafsi wengine mbali na Bw. Ajavon na kwamba Waleta Maombi waliendelea kuwa na maslahi ya

kisheria ya sasa ya kufanya madai yao yachunguzwe. Kwa hivyo, ilitupilia mbali pingamizi hilo.

Kuhusu suala la *res judicata* husika, Mjibu Maombi alidai kwamba hukumu kuhusu fidia katika Maombi Na. 013/2017 isingeweza kuwanufaisha Waleta Maombi, kwani hawakuwa wahusika katika kesi hizo. Waleta Maombi walijibu kwamba hawakuwa wakitafuta kupewa manufaa yanayotolewa na sehemu ya amri ya hukumu hiyo, bali walikuwa wakitegemea hukumu hiyo kama ushahidi unaothibitisha wajibu wa Mjibu Maombi na uhusiano sababishi kati ya ukiukaji ambao tayari umebainishwa na madhara waliyoyapata. Ikirejelea kwamba *res judicata* inahitaji masharti matatu ya pamoja, yaani utambulisho wa wahusika, utambulisho wa maombi na uwepo wa uamuzi wa kwanza kuhusu masuala ya msingi, Mahakama ilibaini kwamba Waleta Maombi hawakuwa walewale katika masuala hayo mawili. Kwa kuzingatia hali ya jumla ya matakwa ya ukubalifu, ilitupilia mbali pingamizi hilo bila kuangalia matakwa mengine mawili.

Kuhusu pingamizi linalotokana na Maombi hayo kutokuafikiana na Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika na Mkataba, Mjibu Maombi alidai kwamba Maombi hayo hayakujumuisha madai mahususi ya ukiukaji wa haki za binadamu, bali yalikuwa mzozo binafsi tu kati ya wanahisa. Mahakama ilibaini kwamba madai ya Waletaji Maombi yalilenga kulinda haki zilizohakikishwa na Mkataba, kwamba hayakujumuisha madai yoyote yasiyoafikiana na Sheria ya Kikatiba na kwamba Maombi hayo yalitimiza matakwa ya Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Kwa hivyo, ilitupilia mbali pingamizi hilo.

Kuhusu pingamizi linalotokana na kushindwa kukamilisha taratibu za ndani za kisheria, Mjibu Maombi alidai kwamba Waleta Maombi hawakuwasilisha suala hilo mbele ya mahakama yoyote ya Benin, hasa Mahakama ya Katiba. Waleta Maombi walidai

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

kwamba Mjibu Maombi kushindwa mara kwa mara kutekeleza hukumu za Mahakama katika Maombi Na. 013/2017 kulionyesha kwamba taratibu za ndani hazikuwa na ufanisi.

Mahakama ilirejelea hukumu zake za kisheria kwamba haitoshi kwa suluhu kuwepo; lazima pia iwe yenye ufanisi, yenye manufaa na kutoa matumaini ya kufanikiwa. Aidha, inaeleza kwamba haitoshi kwa Mleta Maombi kutilia shaka ufanisi wa taratibu za ndani za kisheria bila ushahidi wowote. Lazima achukue hatua zote zinazohitajika ili kuzitumia zote, au angalau kujaribu kuzitumia zote. Mahakama iliangalia upatikanaji na ufanisi wa taratibu za ndani kuhusiana na kila aina ya ukiukaji unaodaiwa kufanywa.

Kuhusiana na madhara waliyoyapata kwa nafasi yao kama wanahisa wa COMON SA, Mahakama ilibainisha kwamba Kifungu cha 1382 na 1383 cha Kanuni ya Madai ya Raia ya Mjibu Maombi na Kifungu cha 48 cha Kanuni ya Madai ya Raia, Biashara, Jamii, Utawala na Hesabu za Fedha kinampa mtu yeyote aliyeumizwa haki ya kufungua kesi ya madai ya fidia mbele ya mahakama ya madai ya raia yenye mamlaka. Iliona kwamba suluhu hiyo ya kawaida ya kisheria, inayopatikana hata kwa wanahisa wa kampuni ambao maslahi yao yanaweza kuwa yameathiriwa na vitendo vya Serikali, ilikuwepo na ilikuwa na uwezo wa kutoa suluhu na kwamba Waleta Maombi walishindwa kuthibitisha kwamba waliitumia au hata kujaribu kuifanya hivyo.

Kuhusiana na kutaifishwa kwa akaunti zao binafsi za benki, Mahakama ilibainisha kwamba Sheria ya Pamoja ya OHADA kuhusu Uandaaji wa Taratibu Rahisi za Urejeshaji na Hatua za Utekelezaji inaweka suluhu mahususi, ambayo inajumuisha kupinga hatua hiyo mbele ya rais wa mahakama inayosikiliza masuala ya dharura (Kifungu cha 49) na, katika suala la kutaifishwa kwa akaunti za benki, kufungua kesi mbele ya mahakama yenye mamlaka ndani ya mwezi mmoja baada ya kujulishwa kuhusu kutaifishwa huko, kwa lengo la kuondolewa hatua hiyo (Kifungu cha 170). Ikirejelea kwamba taratibu za Sheria za Pamoja za OHADA zimejumuishwa katika mfumo wa mahakama wa Mjibu Maombi na kwamba zinajumuisha taratibu za ndani za kisheria, Mahakama iliamua kwamba taratibu hizo za kisheria zilikuwepo, zilifikika

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

na zilikuwa na uwezo wa kukomesha mgogoro. Ilibaini kwamba Waleta Maombi hawakuthibitisha kwamba walilitumia au kwamba kulikuwa na hali mahususi ambazo ziliwazuia kufanya hivyo.

Mahakama ilihitimisha kwamba Waleta Maombi walikuwa na njia za ndani za kisheria zilizokuwepo na zenye ufanisi ambazo hawakuzitumia zote au hata kujaribu kuzitumia zote, kwa hivyo haikuwa tena lazima kuangalia hoja inayohusiana na kuwasilishwa kwa kesi hiyo kwenye Mahakama ya Katiba. Ilibaini kwamba Maombi haya hayakukidhi takwa la ukubalifu chini ya Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama.

Baada ya kubaini kwamba Maombi haya hayakukidhi takwa la Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama na ikirejelea kwamba matakwa ya ukubalifu ni ya jumla, Mahakama iliamua kwamba hakukuwa na haja ya kutoa uamuzi kuhusu uzingatiaji wa matakwa mengine ya ukubalifu. Kwa hivyo, ilitangaza Maombi hayo kuwa hayakubaliki.

Mahakama iliamua kwamba kila upande unapaswa kubeba gharama zake.

Maelezo zaidi

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na maelezo kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inapatikana kwenye tovuti https://ajudata.african-court.org/details-case/0632019.

Kwa maswali mengine yote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe: registrar@african-court.org

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kusikiliza kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki

za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu katika www.african-court.org